FoodShare WISCONSIN

A Recipe for Good Health

Ujumbe Kuhusu Ukaguzi wa Udhibitisho wa Ubora wa FoodShare

INFORMATION ABOUT FOODSHARE QUALITY CONTROL REVIEWS

Je, ukaguzi wa udhibitisho wa ubora wa FoodShare ni nini?

Ukaguzi wa udhibitisho wa ubora wa FoodShare ni ukaguzi wa kesi za FoodShare ili kuhakikisha kwamba shirika lililokuandikisha katika FoodShare lilikupa faida sahihi na linafuata sharia zilizowekwa na serikali ya shirikisho.

Ukaguzi wa udhibiti wa ubora hutumiwa na Idara ya Huduma za Afya ya Marekani (DHS) kuangalia kama:

- Mpango wa FoodShare unaendeshwa kulingana na sheria.
- Shirika lako lilitekeleza kesi lako kisahihi.
- Ujumbe katika faili ya kesi lako ni sahihi.
- Unapokea faida unazostahiki.

Kwa nini kesi yangu ilichukuliwa?

Kesi yako ya FoodShare ilichaguliwa nasibu kwa ukaguzi wa kudhibiti ubora. Ilichaguliwa **sio** kwa sababu bya kitu ulifanya au haukufanya. Kwa kukagua kesi zilizochaguliwa nasibu, DHS inaweza jua iwapo shirika lako linaendesha mpango wa FoodShare kwa usahihi.

Je, ninapaswa kushirikiana?

Sheria ya Shirikisho inasema kwamba lazima ushirikiane na ukaguzi wa kudhibiti ubora. Ikiwa hutatoa taarifa iliyoombwa na ushirikiane na ukaguzi, kesi yako ya FoodShare inaweza kufungwa. Hili likitendeka, utaambiwa muda gani kesi yako inaweza kufungwa.

Je, ni vipi ukaguzi wa hakikisho la ubora wa FoodShare unafanya kazi?

Zifuatazo ni hatua kuu katika mchakato wa ukaguzi wa kudhibiti ubora wa FoodShare:

1. Mtaalam wa udhibiti wa ubora atapewa ukaguzi wa kesi yako ya FoodShare.
2. Mtaalam atapitia faili yako ya FoodShare ili kuona ni hatua gani zilizochukuliwa na shirika la ndani.
3. Baada ya mtaalam kukagua faili ya kesi lako ya FoodShare, atakupigia simu ili kuanzisha mahojiano ya binafsi au ya simu.

   Kumbuka: Ikiwa mhojiwa hawezi kukufikia ili kuanzisha mahijiano, atapeperusha ujumbe kuhusu mahojiano kwako nyumbani pamoja na tarehe na wakati wa mahojiano. Taarifa ya mahojiano itakuwa na nambari ya simu ili uweze kupiga simu na kuanzisha upya mahojiano yako, ikiwa ni lazima.

4. Kama sehemu ya mahojiano, utaombwa kusahihi fomu ya habari ya kuachiliwa iliyoandikwa. Fomu hii inatoa kibali cha wataalam kuwasiliana na vyanzo vingine (kama vile mabenki, wamiliki wa nyumba, au waajiri) ili kuthibitisha habari uliyotoa kwa usajili wa FoodShare yako. Vyanzo hivi

vinaweza kuulizwa kutoa habari, kama vile taarifa na ushahidi wa ajira.

Kumbuka: Kulingana na sheria ya serikali, mtu yeyote, taasisi ya kifedha, shirika la ripoti ya mikopo, muajiri, au shule imeidhinishwa kutoa taarifa kwa usajili wako wa FoodShare.

Je, ni nini inayofanyika baada ya ukaguzi wa dhibitisho la ubora wa FoodShare?

Pindi tu mahojiano yako yamekamilika na mtaalam amakagua ujumbe wote kutoka faili ya kesi lako la FoodShare, rekodi zako binafsi, na vyanzo vingine, uamuzi utafanywa iwapo faida zako za FoodShare zilitolewa kikamilifu. Iwapo makosa yatapatikana katika faida zako, utajulishwa na shirika lako kuhusu mabadiliko yoyote katika faida.

Utakuwa na haki ya kukata rufaa mabadiliko yoyote kwa faida au adhabu yoyote ya kutoshirikiana na ukaguzi wa kudhibiti ubora. Utapata taarifa kuhusu kukata rufaa ikiwa hatua yoyote ya hizi hutokea.

Matokeo ya ukaguzi wako wa kudhibiti ubora hupelekwa Idara ya Kilimo Chakula na Lishe nchini U.S.

Je, itanilazimu kufanya ukaguzi mwingine wa kudhibiti ubowa wa FoodShare?

Wataalam wa udhibiti wa ubora wa Serikali wataangalia mapitio mengine ambayo yamechaguliwa kwa nasibu. Uhakikisho upya ni kesi tayari iliyopitiwa na hali iliyochaguliwa kwa ajili ya ukaguzi kupitia serikali ya shirikisho. Ikiwa kesi yako imechaguliwa kwa nasibu, unaulizwa ushirikiane na wakaguzi wa shirikisho wakiwasiliana na wewe.

Je, ujumbe wangu ni wa siri?

Taarifa unampa mkaguzi wa serikali au shirikisho itatumiwa na wafanyakazi ambao wanaendesha mipango ya msaada ili kuamua hali ya wafanyakazi wengine walioidhinishwa na sheria.

Una haki ya:

- Kuangalia maelezo yote ya umma na ya kibinafsi yaliyokusanywa kukuhusu.
- Changamoto ukweli katika kesi yako unazoamini sio sahihi au kamili.
- Angalia faili ya kesi yako yote, ila kwa aina fulani za habari ambazo zinawekwa kuwa siri kisheria.

Je, ni wapi naweza pata ujumbe zaidi?

Faili hii ya ukweli ina taarifa ya jumla kuhusu ukaguzi wa ubora wa FoodShare. Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na mkaguzi kwa nambari uliyopewa katika ujumbe wa mahojiano yako. Ikiwa huwezi kupata mwongozo wako, piga simu 608-261-8321.

Taarifa ya Kutobagua ya USDA

Kwa mujibu wa Sheria Shirikisho za Kiraia na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), kanuni za haki za kiraia na sera, USDA, wakala zake, ofisi, na waajiriwa, na taasisi zinazoshiriki kwa au kupa mipango ya USDA zinakatazwa kubagua kulingana na uraia, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, imani ya kidini, ulemavu, umri, imani ya kisiasa, au dhahabu au kulipiza kisasi kwa shughuli za kipaumbele za haki za kiraia kwa mpango wowote au shughuli yoyote iliyofanywa au fadhiliwa na USDA.

Watu walio na ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliiano kwa taarifa ya programu (km., Braille, kuchapisha kubwa, kanda ya susikiliza, Lugha ya Ishara ya Marekani, n.k), wanapaswa kuwasiliana na Shirika (Jimbo au eneo) ambapo waliomba faida. Watu ambao ni viziwi, ungumu wa kisikia, au wana ulemavu wa kuongea wanaweza wasilina na USDA kupitia Huduma ya Usambazaji wa Shirikisho kwa (800) 877-8339. Zaidi ya hayo, maelezo kuhusu mpango yanaweza kupatikana kwa lugha zingine kuliko Kiingereza.

Ili kufungua mpangao wa malalamishi ya ubaguzi, kamilisha Fomu ya Mpango wa Malalamishi ya Ubaguzi ya USDA, (AD-3027) inayopatikana kwa mtandao kwa: Jinsi ya kufungua Malalamishi, na katika ofisi yoyote ya USDA, au kuandika barua kwa USDA na kutoa katika hiyo barua maelezo yote yaliyoulizwa. Kuomba nakala ya fomu ya malalamishi, piga simu (866) 632-9992. Tuma fomu yako kamili au barua kwa USDA kwa:

(1) barua: U.S. Department of Agriculture
Office of the Assistant Secretary for Civil Rights
1400 Independence Avenue, SW
Washington, D.C. 20250-9410;

(2) faksi: (202) 690-7442; au

(3) barua pepe: program.intake@usda.gov.

Taasisi hii ni mtoa fursa sawa.